WIZARA YA NISHATI

# NewsBulletin

## HABARI ZA NISHATI




# RAIS MWINYI ATEMBELEA BANDA LA NISHATI MAONESHO YA SABASABA

WIZARA YA NISHATI +255-26-2320148 AU +255-26-232018

WIZARA YA NISHATI

# BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**
Mhandisi Felchesmi Mramba

**MAKAMU MWENYEKITI**
Dkt. James Mataragio
Dkt. Khatibu Kazungu

**MHARIRI**
Neema Chalila Mbuja
Teresia Mhagama

**WAANDISHI**
Timotheo Mathayo
Zuwena Msuya
Immaculate Makilika
Felista Charles

**WAPIGA PICHA**
Henry Kilasila
Godfrey Mwemezi
Ruben Richard
Amanzi Kimonjo
Mustafa Shahame

**MSANIFU KURASA**
Brian Mbaga

© NISHATI 2025

# RAIS MWINYI ATEMBELEA BANDA LA NISHATI MAONESHO YA SABASABA

- Apatiwa elimu juu ya utekelezaji wa mkakati wa Taifa wa Nishati safi ya kupikia
- Wizara ya Nishati kuendelea kuweka mazingira mazuri kwa tasisi zake kutekeleza majukumu yake kikamilifu




Mkuu wa kitengo cha Mawasiliano Serikalini Bi Neema Chalila Mbuja, alimweleza Rais wa Zanzibar na mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi juu ya hatua za utekelezaji zilizofikiwa kwenye utekelezaji wa mkakati wa Taifa wa nishati safi ya kupikia na kuongeza kuwa ajenda hiyo ni utekelezaji wa azimio la Mhe Rais Samia kama kinara wa nishati safi ya kupikia.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt Hussein Ali Mwinyi mnamo tarehe 7 Julai, 2025 alitembelea banda la Wizara ya Nishati kwenye Monesho ya Biashara ya Kimataifa maarufu kama SABASABA jijini Dar es salaam.

Akiwa kwenye Banda la Wizara ya Nishati, Mhe. Mwinyi alipokelewa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Bi Neema Chalila Mbuja, ambapo alimweleza juu ya hatua za utekelezaji zilizofikiwa kwenye utekelezaji wa mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia na kuongeza kuwa ajenda hiyo ni utekelezaji wa azimio la Mhe. Rais Samia kama kinara wa nishati safi ya kupikia.

Amesema Wizara ya Nishati kupitia taasisi zilizopo chini ya Wizara zimekuwa zikitekeleza kwa vitendo ajenda hiyo kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan ambae ni kinara wa nishati safi ya kupikia kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2034 asilimia 80 ya watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia.

Wizara ya nishati tayari imezindua mikakati miwili ya nishati safi ya kupikia na ule wa mawasiliano ili kuwezesha utekelezaji wa ajenda ya nishati safi ya kupikia kwa vitendo.

# DKT. BITEKO ASHIRIKI MKUTANO WA NYUKLIA AFRIKA

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt Doto Biteko mnamo tarehe 29 Juni, 2025 amehudhulia Mkutano unaohusu masuala ya nyuklia Afrika uliofanyika Nchini Rwanda.

Katika Mkutano huo uliofanyika kuanzia tarehe 30 Juni hadi 1Julai, 2025 nchini humo umejumuisha wadau mbalimbali wa nishati kutoka ndani na nje ya Afrika wenye lengo la kuharakisha matumizi ya nyuklia kwa kutumia teknolojia ya kisasa ili kuleta mabadiliko ya nishati Afrika.

Aidha, katika Mkutano huo Dkt. Biteko aliambatana na Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mhe. Cosato Chumi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba na Mkurugenzi wa Tume ya Mionzi ya Atomiki, Prof. Najat Mohamed.





# TANZANIA INAYO UMEME WA KUTOSHA – DKT.BITEKO



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kutembelea Kituo cha kuzalisha umeme cha Kinyerezi Julai 10, 2025 jijini Dar es salaam (Picha na ONWM & WN)


Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema Tanzania ina umeme wa kutosha baada ya kukamilika kwa Miradi mikubwa ya uzalishaji umeme ukiwemo Mradi wa Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP ) ambao pekee unazalisha Megawati 2115.

Naibu Waziri Mkuu ameyasema hayo mnamo tarehe 10 Julai, 2025 wakati wa ziara yake.ya kukagua ya miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia ya Kinyerezi I, Kinyerezi I Extension na Kinyerezi II Jijini Dar esSalaam.

Amesema licha ya kazi kubwa inayofanywa na TANESCO baadhi ya maeneo yalikabiliwa changamoto ya upatikanaji wa umeme lakini mpaka sasa yameendelea kuimarika.

Dkt. Biteko amefafanua kuwa upatikanaji wa umeme unaendana na mahitaji ya ongezeko la watu na TANESCO inatarajia kuongeza uzalishaji umeme katika Kituo cha Kinyerezi III kutoka megawati 600 katika mpango wa awali hadi kufika Megawati 1000.

‘’Nataka niseme mbele yenu ndugu zangu, Mhe. Rais Samia ndio Kinara wa kufanya haya yote yafanikiwe amefanya uwekezaji mkubwa kwenye



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akishuhudia uzalishaji wa umeme kupitia vifaa maalum vinavyoonesha uzalishaji huo mara baada ya kutembelea Kituo cha kuzalisha umeme cha Kinyerezi Julai 10, 2025 jijini Dar es salaam.

alisisitiza Dkt. Biteko.

Vilevile, Dkt. Biteko ametembelea Kituo cha Kupokea Gesi Asilia Kinyerezi kwa ajili ya kukagua miundombinu ya kusafirisha gesi na kuwataka kuongeza uzalishaji wa gesi ili kusaidia kukidhi ongezeko la mahitaji ya umeme.

Katika ziara hiyo Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko aliongozana na viongozi mbalimbali akiwemo katibu Mkuu wa Wizara ya nishati Mha. Felchesmi Mramba, Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mhe.Edward Mpogolo na Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO Bw. Lazaro Twange.

Sekta ya Nishati na ndio maana kwenye bajeti iliyopita Wizara hii imepata Shilingi Trilioni 2.3 kikubwa anataka wananchi wapate umeme wa uhakika," alisema Dkt Biteko.

Aidha, Naibu Waziri Mkuu pia ametumia nafasi hiyo kuipongeza TANESCO kwa maboresho makubwa yanayoendelea kufanyika ya kuwahudumia wateja hasa kwa uharaka wao wa kukabiliana na dharula zozote za umeme zinazojitokeza.''Kuna maboresho makubwa yamefanyika katika kuwahudumia wananchi naona jitihada kubwa zinafanyika, mmekuwa na uharaka wa kushughulikia changamoto za umeme lakini pia niwapongeze kwa kuimarisha Kituo cha miito ya simu sasa wananchi wanahudumiwa bila gharama yoyote,"



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akikagua mitambo mbalimbali ya umeme wa Gesi mara baada ya kutembelea Kituo cha kuzalisha umeme cha Kinyerezi Julai 10, 2025 jijini Dar es salaam (Picha na ONWM & WN)

# PROF. MWANDOSYA KINARA WA MATIBABU YA SARATANI NCHINI - DKT. BITEKO

- Dkt. Biteko azindua Kitabu cha Living with Cancer cha Prof. Mark Mwandosya
- Watanzania watakiwa kujenga utamaduni wa kupima afya
- Serikali yaimarisha huduma za uchunguzi na matibabu ya saratani



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko(wa pili kulia), akizindua Kitabu: Living with Cancer, kilichoandikwa na Prof. Mark Mark Mwandosya ( mwenye shati jeupe). Kushoto ni Mke wa Prof. Mwandosya-Lucy, Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mkuki na Nyota publishers.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amemuelezea Prof. Mark Mwandosya kuwa ni Shujaa wa Saratani ya Damu (Multiple Myeloma) ambaye ameishi na Saratani kwa zaidi ya miaka 14.

Dkt. Biteko amesema hayo katika uzinduzi wa kitabu cha Maisha ya Mgonjwa anayeishi na Saratani ya Damu Multiple Myeloma (Living with Cancer: Diaries of Multiple Myeloma Patient) kilichoandikwa na Prof. Mark Mwandosya ambaye ni msomi, mwandishi na mwanasiasa wa muda mrefu nchini.

"Katika miaka 14 ya kishujaa, Prof. Mwandosya amekuwa shuhuda kwetu sote kuwa endapo utafuata hatua stahiki za matibabu, unaweza kupona saratani na kuendelea kuishi maisha bora. Asante sana na hongera sana Profesa. Mwenyezi Mungu azidi kukubariki," Amesema Dkt. Biteko.

Amesema kupitia historia ya Prof. Mwandosya ya matibabu yake ya saratani Kitabu hicho kitasaidia kunusuru maisha ya watanzania wengi ambao wangeweza kushindwa kunufaika na huduma za matibabu kwa kukosa taarifa sahihi.

"Nakupongeza sana tena Profesa kwa kujitoa kuwa sehemu ya ushuhuda ili watanzania na Dunia ijifunze kupitia maisha yako. Hakika huu ni upendo wa hali ya juu kwa nchi yako. Nami kwa niaba ya Serikali nakupongeza kwa uamuzi wako huu. Aidha, ninakuombea kwa Mungu akupe afya njema na maisha marefu zaidi na zaidi, " Amesema Dkt. Biteko.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akimuelezea Prof. Mark Mwandosya kuwa ni Shujaa wa Saratani ya Damu ambaye ameishi nayo kwa zaidi ya miaka 14 katika uzinduzi wa kitabu cha Maisha ya Mgonjwa anayeishi na Saratani ya Damu Multiple Myeloma (Living with Cancer: Diaries of Multiple Myeloma Patient) kilichoandikwa na Prof. Mark Mwandosya ambaye ni msomi, mwandishi na mwanasiasa wa muda mrefu nchini.

Amesema kuwa, saratani ni ugonjwa ambao unaweza kudhibitiwa au kutibiwa na kupona kabisa endapo mgonjwa atapata matibabu kwa wakati na kumshukuri Profesa Mwandosya kwa kuamua kuwa miongoni mwa watu wanaoleta suluhisho la tatizo hili kwa jamii.

Kwa upande wake, Prof. Mwandosya amesimulia safari yake ya kuishi na ugonjwa wa Multiple Myeloma, aina adimu ya saratani ya damu inayodumu kwa muda mrefu. Amesema kupitia ugonjwa huo ameamua kueleza changamoto na mafunzo ya kimwili, kiakili na kiroho aliyopitia akisisitiza ujumbe wa matumaini, ujasiri na heshima katika maisha.

"Ugunduzi wa Saratani haupaswi kuchukuliwa kama hukumu ya kifo ni safari ya kuendelea kuishi na kutafuta maana na nguvu hata katikati ya maradhi, amesema Prof. Mwandosya.

Naye, Mtaalamu wa magonjwa ya damu na mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Dkt. Clara Chamba ametoa rai kwa watanzania kufanya uchunguzi wa afya mapema na kupenda kufanya mazoezi

Katika kupambana na Saratani, Serikali kupitia Wizara ya Afya imefanya uwekezaji mkubwa katika huduma za uchunguzi na matibabu ya saratani na magonjwa mengine kwa ujumla.

# TUNAWEZA KUZUIA ASILIMIA 80 YA VIFO NCHINI TUKIBADILI MTINDO WA MAISHA-DKT.BITEKO

- Asisitiza kuhusu mazoezi ya mwili ili kujikinga na maradhi yasiyoambukiza
- Apongeza NBC Dodoma Marathon kuiunga mkono Serikali mapambano dhidi ya Saratani ya Shingo ya kizazi na kusomesha Wataalam wa Afya
- Apongeza Kampeni ya MTU NI AFYA inayohamasisha Watanzania kufanya mazoezi
- NBC Dodoma Marathon yawezesha matibabu ya Saratani ya Shingo ya Kizazi kwa Wanawake 4800; mafunzo kwa Wakunga 100 na kuchangia ujenzi wa wodi



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko akipongeza Benki ya NBC kupitia NBC Dodoma Marathon kwa kuunga mkono Serikali katika nyanja mbalimbali ikiwemo Sekta ya Afya kwani katika mwaka 2025 Marathon hiyo imelenga kuendeleza mapambano dhidi ya Saratani ya shingo ya kizazi.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko amesema kuwa asilimia 80 ya vifo nchini vinaweza kuzuilika endapo Watanzania wataamua kubadili mtindo wa maisha ikiwemo kuwa na utaratibu wa kufanya mazoezi ya mara kwa mara.

Amesema hayo jijini Dodoma wakati akimwakilisha Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa katika kilele cha msimu wa Sita wa NBC Dodoma Marathon 2025 ambayo imelenga kukusanya fedha kwa ajili ya kuokoa afya ya mama na mtoto.


"Taarifa ya Shirika la Afya Duniani ya mwaka 2022, inaeleza kuwa, mazoezi ya mara kwa mara kama vile kukimbia, yana uwezo wa kupunguza hatari ya ugonjwa wa moyo kwa zaidi ya asilimia 35.Vile vile, mazoezi ya mwili husaidia kujikinga na magonjwa mengine yasiyoambukiza kama vile kisukari, shinikizo la damu, saratani na magonjwa mengine mengi." Ameeleza Dkt. Biteko

Kwa upande wa Tanzania, Dkt. Biteko amesema kuwa asilimia 33 ya Watanzania watu wazima wana uzito uliopitiliza na asilimia 28 wana shinikizo la damu ambapo ameeleza kuwa magonjwa hayo yanachangia zaidi ya asilimia 40 ya vifo vya mapema lakini asilimia 80 ya vifo hivyo vinaweza kuzuilika kwa kubadili mtindo wa maisha.

Dkt. Biteko ameipongeza Benki ya NBC kupitia NBC Dodoma Marathon kwa kuunga mkono Serikali katika nyanja mbalimbali ikiwemo Sekta ya Afya kwani katika mwaka 2025 Marathon hiyo imelenga kuendeleza mapambano dhidi ya Saratani ya shingo ya kizazi kwa kushirikiana na Taasisi ya Saratani ya Ocean Road.

Pia, imelenga kutoa ufadhili wa masomo ya Wakunga kupitia Taasisi ya Benjamin Mkapa ili kusaidia kupunguza vifo vya mama na mtoto wakati wa uzazi na kutoa ufadhili kwa mafunzo ya Wauguzi Maalum wa kusaidia watoto wenye changamoto ya usonji (Autism), kwa kushirikiana na AMREF Afrika.

Vilevile, Dkt. Biteko amesema kuwa tangu NBC Dodoma Marathon kuanzishwa mwaka 2020 imekuwa ni moja ya vilelezo vya kujenga mshikamano,



uzalendo wa kweli na kutatua matatizo mbalimbali katika jamii ikiwemo changamoto za kiafya.

Dkt. Biteko ameipongeza NBC Dodoma Marathon kwa kuendelea kuimarika kwani mwaka 2024 ilihusisha washiriki 8,000 na mwaka huu imekuwa na washiriki zaidi ya 12,000 sawa na ongezeko la zaidi ya asilimia 50.

Vile vile, mwaka 2024 NBC Dodoma Marathon ilikusanya kiasi cha Shilingi Milioni 300 huku mwaka 2025 ikikusanya kiasi cha Shilingi Milioni 700 sawa na ongezeko la mapato ya zaidi ya asilimia 133.33.

Amesema kuwa, Serikali itaendelea kushirikiana na wadau kama NBC ambao wameendelea kutumia mashindano ya mbio kuimarisha afya za wananchi na kuchangia masuala mbalimbali ya kijamii ikiwemo kuokoa afya za watu.

Katika hatua nyingine, Dkt. Biteko ametoa rai kwa Wizara ya Afya, Serikali za Mitaa, Mashirika ya kiraia, Sekta binafsi na wananchi wote kufanya mbio na mazoezi kuwa sehemu ya maisha ya kila siku ili kuweza kujikinga na matatizo ya afya ambayo wananchi wanaweza kuyapata.

"Nitashukuru sana kusikia kila Taasisi imetenga kwa uchache siku moja kwa mwezi ili kuwa na mazoezi ya pamoja, hii itasaidia kuimarisha afya zetu na kujenga Taifa Imara. " Amesisitiza Dkt. Biteko

Vilevile ameipongeza Wizara ya Afya, kwa Kampeni ya MTU NI AFYA ambayo inawahamasisha Watanzania kufanya mazoezi kwa angalau dakika 30 kila siku, kula lishe bora, kupima afya mara kwa mara na kujiepusha na tabia hatarishi.

Kwa upande wake, Mhe. Profesa Palamagamba Kabudi, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo amesema mbio za NBC Dodoma Marathon zimekuwa kivutio kwa wanamichezo wengi kushiriki kutokana na kundaliwa vizuri ambapo amesema kuwa Wizara hiyo itaendelea kuiunga mkono benki ya NBC katika maandalizi ya mbio hizo ambazo zimekuwa na matokeo chanya.

Amesema Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo itaendelea kuweka mazingira mazuri ya wananchi kushiriki michezo mbalimbali pamoja na kuendelea kujenga viwanja vya michezo katika maeneo mbalimbali ikiwemo Arusha, Dodoma na Dar es Salama ili kuwezesha vijana kujiimarisha kimichezo na kiafya.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi alisema NBC Marathon imekuwa ni moja ya alama za sekta binafsi katika kuwekeza kwenye sekta ya afya na nyinginezo, akieleza kuwa katika kipindi cha miaka mitano mbio hizo zimefanikiwa kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 1, ambazo zimekuwa na mchango mkubwa katika Sekta ya Afya.

Ametaja mafanikio ya marathon hiyo kuwa ni pamoja na kutoa elimu na kufanikisha kupimwa Saratani ya shingo ya kizazi kwa Wanawake zaidi ya 200,000 na kufadhili matibabu kwa wagonjwa 4,800 waliogunduliwa na kansa hiyo katika Hospitali ya Ocean Road.

Amesema, NBC Dodoma Marathon imetoa ufadhili kwa Wakunga 100 katika chuo cha Wakunga Morogoro kwa ushirikiano na Taasisi ya Benjamin Mkapa Foundation huku lengo likiwa ni kufadhili wakunga 500 ifikapo 2028.

Pia ameeleza kuwa, NBC Dodoma Marathon imechangia ujenzi wa Wodi maalum ya Wanawake katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na maeneo mengine katika maendeleo ya sekta ya afya.

Amesema msimu wa sita wa NBC Dodoma Marathon umehusisha wakimbiaji 12,000 na wamefanikiwa kukusanya shilingi milioni 700 kwa ajili ya afya ya mama na mtoto ikilenga kuwapatia uchunguzi wa mwanzo wa saratani ya kansa ya kizazi wanawake 10,000, kutoa ufadhili kwa wakunga 100 na kuanzisha mpango mpya wa masomo kwa wauguzi 100 watakaoshughulika na watoto wenye changamoto ya usonji.

NBC Dodoma Marathon 2025 iliyokuwa na kaulimbiu ya Kata Wese Okoa Maisha imehusisha wanariadha kutoka ndani na nje ya nchi ambapo washindi wamepewa zawadi za jumla ya shilingi milioni 80. Aidha imekabidhi pikipiki 10 kwa Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma.

# BENKI YA DUNIA KUJENGA MRADI WA NJIA YA KUSAFIRISHA UMEME WA KV 400 KUTOKA UGANDA HADI TANZANIA

- Yakutana na Mhandisi Mramba kueleza uamuzi huo baada ya kujiridhisha kuwa hauna athari kimazingira
- Yaialika Wizara ya Nishati kushiriki Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa jijini New York
- Mramba aahidi kuendelea kushirikiana na Benki ya Dunia utekelezaji miradi ya Nishati



Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mha. Felchesmi Mramba (wa pili kushoto), Mtaalam wa Nishati kutoka Ofisi ya Benki ya Dunia nchini Tanzania Dkt. Rhonda Jordan (wa pili kutoka kulia), Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga (wa kwanza kulia) na Mhandisi Mkuu wa Nishati, John Magheni wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kufanya mazungumzo katika Ofisi za Wizara ya Nishati Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma Julai 23, 2025

Benki ya Dunia (WB) imeeleza kuwa itatoa fedha za utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo mkubwa wa kilovolti 400 kutoka nchini Uganda hadi Tanzania.

Hayo, yameelezwa na Mtaalam wa Nishati kutoka Ofisi ya Benki ya Dunia nchini Tanzania, Dkt. Rhonda Jordan wakati alipofanya mazungumzo na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mha. Felchesmi Mramba katika Ofisi za Wizara ya Nishati Mji wa Serikali Mtumba Julai, 23 Jijini Dodoma.

Dkt. Rhonda amesema kuwa kwa sasa benki hiyo imeridhia kutekeleza mradi huo baada ya kujiridhisha kuwa hauna athari za kimazingira kama ilivyokuwa ikielezwa hapo awali.

“Bodi ya Wakurugenzi sasa itapitisha fedha kwa ajili ya kuanza kutekeleza mradi huo, ambao ulikuwa ukisuasua kutekelezwa kwa madai ya kuathiri mazingira, lakini sasa bodi imeridhika na itatoa fedha za kuanza kuutekeleza”, amesema Dkt. Rhonda

Katika hatua nyingine, Dkt. Rhonda ameialika Wizara ya Nishati kushiriki katika Mkutano wa Umoja wa Mataifa utakaofanyika Jijini New York nchini Marekani mwezi Semptemba, 2025.

Katika mazungumzo yao, Katibu Mkuu Mramba amemueleza Dkt.Rhonda kuwa wataendelea kushirikiana na Benki ya Dunia katika miradi mbalimbali ya Nishati ikiwemo ule wa usafirishaji umeme wa Tanzania-Zambia (TAZA) na mingine inayofafana kama hiyo. Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mha. Innocent Luoga na Mhandisi Nishati Mkuu John Mageni.

# LUKUVI AIPONGEZA WIZARA YA NISHATI KUTEKELEZA AZMA YA SERIKALI YA KUHAMIA KATIKA MJI WA SERIKALI MTUMBA

- Aishukuru Wizara kwa kumheshimisha Dkt.Samia Suluhu Hassan
- Ampongeza Dkt. Biteko kwa kuweka msukumo wa Watumishi kuhamia Mtumba.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu, Mhe. William Lukuvi akitembelea jengo la Wizara ya Nishati katika Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma. Kulia kwake ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba.

Wizara ya Nishati imepongezwa kwa kuhamia rasmi katika Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma ambapo Idara na Vitengo vyote vya Wizara sasa vimeshahamia katika jengo la Wizara lililopo katika Mji huo wa Serikali.

Pongezi hizo zimetolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu, Mhe. William Lukuvi wakati alipotembelea jengo la Wizara katika Mji wa Serikali Mtumba ambapo alipokelewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Naibu Katibu Mkuu, Dkt. James Mataragio pamoja na Menejimenti ya Wizara.

"Nakupongeza sana Katibu Mkuu kwa hatua hii, pamoja na Mkandarasi wa Jengo na Msimamizi, pia nawapongeza kwa nia thabiti ya kuhamia katika Mji huu wa Serikali baada ya Mhe. Rais Samia kutoa fedha zilizowezesha ujenzi wa majengo haya Serikali Mtumba". Amesema Mhe. Lukuvi

Ameongeza kuwa, nia ya Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma kwa ufanisi katika eneo moja na hivyo kuondoa usumbufu wa kutumia muda mrefu kupata huduma katika maeneo tofauti.

' Nawashukuru sana Wizara kwa kumheshimisha Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu nia yake ni Watumishi kuwa pamoja katika utoaji wa huduma ili kuleta ufanisi." Amesema Mhe. Lukuvi

Amempongeza pia Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko kwa kuweka msukumo kwa Wizara katika kukamilisha jengo hilo na kwa watumishi kuhamia katika jengo husika.

Aidha Mhe. Lukuvi ametoa rai kwa watumishi wa Wizara kuhakikisha wanatunza vyema miundombinu na vifaa vilivyopo ili viweze kudumu kama ilivyokusudiwa.

# SEKTA YA NISHATI IWE KICHOCHEO CHA KUIUNGANISHA AFRIKA KUJENGA UCHUMI

Mawaziri wanaoshughulikia masuala ya Nishati na Maji wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wametaka Sekta ya Nishati kuwa kichocheo cha kuiunganisha Afrika katika kujenga uchumi wake.

Wamesema hayo mnamo tarehe 4 Julai 2025 wakati wakihitimisha mkutano wa SADC jijini Harare nchini Zimbabwe ambao ulilenga kuimarisha na kujadili masuala mbalimbali yatakayowezesha mtangamano wa Kikanda katika sekta za nishati na maji.

Akizungumza wakati akihitimisha mkutano huo, Waziri wa Nishati na Maendeleo ya Umeme wa Zimbabwe, Mhe. Dkt. July Moyo, ameitaka jumuiya hiyo ya SADC kuipa kipaumbele sekta ya nishati na maji ili kuifanya kuwa na tija kwa wananchi katika kukuza uchumi wao kwa kuwa nishati ni chanzo kikubwa cha maendeleo.

Aidha, ameipongeza Tanzania kwa kuandaa na kuwa mwenyeji wa kufanikisha Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Nishati Afrika wa Misheni 300 (M300) ambao ulifanyika kwa mafanikio. Pia, Dkt. Moyo amezishukuru Nchi wanachama zilizohudhuria katika mkutano huo muhimu uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Kwa upande wake, Waziri wa Nishati wa Malawi, Mhe. Ibrahim Matola ameitaka SADC kuhakikisha inaiendeleza miradi yote ya kipaumbele katika jumuiya ili kuifanya sekta ya nishati kuwa kimbilio katika kujenga uchumi wa nchi zao.




Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga alipohudhuria mkutano huo wakati wakihitimisha mkutano wa SADC jijini Harare nchini Zimbabwe ambao ulilenga kuimarisha na kujadili masuala mbalimbali yatakayowezesha mtangamano wa Kikanda katika sekta za nishati na maji.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga ameitaka SADC kuhakikisha inakuwa na mikakati madhubuti ya utekekezaji wa maazimio mbalimbali wanayofikia katika makongamano ya umoja huo ili yawe na tija kwa wananchi na taifa kwa ujumla na kuifanya sekta ya nishati kuwa chachu na mkombozi ndani ya SADC.

Kuhusu utekelezaji wa nishati safi ya kupikia katika jumuiya hiyo, Mhe. Kapinga ameitaka SADC kuweka dhamira thabiti na mikakati madhubuti ya utekelezaji wa ajenda ya nishati safi ya kupikia ili kuwafikia watu wengi zaidi katika SADC.

Mkutano huo uliohitimishwa leo, umehudhuliwa na Balozi wa Tanzania nchini Zimbabwe, Mhe. Suzan Kaganda, Wataalam mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati akiwemo Kamishna Msaidizi wa Maendeleo ya Umeme, Mha. Styden Rwebangila, Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mha. Hassan Saidy, Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji (TPDC), Derick Moshi, Mkurugenzi wa Mifumo ya Udhibiti Umeme (TANESCO) , Mha. Deogratius Mariwa, Mkurugenzi wa Udhibiti Uchumi (EWURA), Msafiri Mtepa na Wataalam kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

# DKT KAZUNGU AKUTANA NA WAWEKEZAJI KUTOKA JAPAN, WAAHIDI KUWEKEZA KWENYE MIRADI YA UMEME

- Pia kuwekeza kwenye miundombinu ya usafirishaji umeme nchini
- Waialika Tanzania kushiriki mkutano wa Tisa wa maendeleo kati ya Japan na Afrika
- Waupongeza mpango mahsusi wa Nishati wa Taifa kuwa bora na wa mfano kwa nchi za Afrika




Naibu katibu Mkuu Wizara ya Nishati, anayeshughulikia umeme na nishati jadidifu Dkt Khatibu Kazungu (wa tatu Kulia), katika picha ya Pamoja wawekezaji kutoka nchini Japan kupitia kampuni ya Toyota Tshusho Cooperation, baada ya kufanya mazungumzo kuhusu uwekezaji wa miradi mbalimbali kwenye sekta ya umeme hususan umeme wa jua, upepo na njia za kusafirisha umeme pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme chini ya mpango mahsusi wa Nishati wa Taifa ujulikanao kama Energy Compact.

Naibu katibu Mkuu Wizara ya Nishati, anayeshughulikia umeme na nishati jadidifu Dkt Khatibu Kazungu, alikutana na kuzungumza na wawekezaji kutoka nchini Japan kupitia kampuni ya Toyota Tshusho Cooperation, uliolenga kufanya mazungumzo kuhusu uwekezaji wa miradi mbalimbali kwenye sekta ya umeme hususan umeme wa jua, upepo na njia za kusafirisha umeme pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme chini ya mpango mahsusi wa Nishati wa Taifa ujulikanao kama Energy Compact.

Kupitia serikali ya Japan chini ya Japan International Banking Corporation, Japan imeonesha nia yake ya kuwekeza kwenye maeneo hayo na kwa sasa wapo kwenye mazungumzo na Serikali ya Tanzania ili kuainisha maeneo hayo ya uwekezaji.

Dkt Kazungu amesema Japan imeonesha nia hiyo ya kuwekeza chini ya mpango huo mahsusi kutokana na Tanzania kuwa na mpango mzuri wa ajenda ya Compact ambao umekuwa wa mfano kwa nchi za Afrika hususan kwenye mafanikio kuunganisha umeme kwa wateja, na nchi nyingi za Afrika zimekuwa zikijifunza kutoka mpango wa Tanzania.

Mpango mahusus wa Nishati wa Taifa ulibuniwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Benki ya Dunia kwa lengo la kuzisaidia nchi za Afrika kutekeleza miradi mbalimbali ya nishati wakati wa mkutano wa wakuu wa nchi uliofanyika jijini Dar es salaam wa Mission 300 uliobeba ajenda ya kuhakikisha waafrika milioni 300 wanafikiwa na umeme ifikapo mwaka 2030.

Katika hatua nyingine Serikali ya Japan imeialika Tanzania kushiriki kwenye mkutano wa tisa wa masuala ya maendeleo kwa nchi za Afrika utakaofanyika nchini Japan mwezi Agosti, 2025 kwa lengo la kuzikutanisha nchi za Afrika kujadili masuala ya maendeleo kwenye sekta mbalimbali.

# NISHATI SAFI YA KUPIKIA NI AJENDA YA DUNIA, WIZARA INAITEKELEZA KWA VITENDO - DKT. KAZUNGU

- Apokea Magari Mawili kutoka Umoja wa Ulaya kwa ajili ya kuanza kampeni ya kutoa elimu ya uhamasishaji wa nishati safi ya kupikia nchi nzima
- Amshukuru Dkt Samia kwa kuwa kinara wa nishati safi na kuibeba ajenda hiyo
- Umoja wa Ulaya waridhishwa na jitihada za Tanzania kwenye kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia
- UNCDF yaahidi kushirikiana na Wizara kuhakikisha watanzania wanafikiwa na elimu ya nishati safi




Naibu katibu Mkuu Wizara ya Nishati anayeshughulikia umeme na nishati Jadidifu, Dkt Khatibu Kazungu mnamo tarehe 04 Julai, 2025 amepokea magari mawili yatakayotumika kwa ajili ya kampeni ya kuhamasisha na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia chini ya kampeni ya nishati safi ya kupikia Okoa Maisha na Mazingira itakayoendeshwa nchi nzima na Wizara ya nishati kwa kushirikiana na UNCDF.

" Ajenda ya Nishati safi ya kupikia ni ajenda ya Dunia na sisi Wizara ya Nishati tuko tayari kwa utekelezaji ili kumuunga mkono Mhe. Rais Samia" Amesema Dkt. Kazungu

Aidha, ameishukuru Umoja wa Ulaya, na UNCDF kwa kutekeleza mradi wa nishati safi ya kupikia chini ya mfuko wa Cook fund kwa kuwa umesaidia kubadili maisha na mitazamo ya wananchi kuhusu utekelezaji wa miradi ya Nishati safi.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Balozi wa Umoja wa Ulaya Mhe. Balozi Christine Grau amesema umoja wa Ulaya uko tayari kuendelea kuisaidia Tanzania kwenye utekelezaji wa Nishati safi ya kupikia na tayari EU imetoa kiasi cha Euro Milioni 19.4 sawa na shilingi Bilioni 59 kutekeleza

miradi ya nishati safi ya kupikia kwa mikoa ya Dar es salaam, Dodoma, Pwani, Morogoro na Mwanza.

Kuhusu magari amesema magari hayo mawili yana thamani ya Euro 130,000 na amewataka Wizara ya Nishati kuhakikisha wananchi wa vijijini wanafikiwa na nishati safi ya kupikia

Tanzania inajipanga kutekeleza kwa vitendo mkakati wa Taifa wa Nishati safi ya kupikia chini ya mkakati wa Mawasiliano wa Taifa ili kutoa elimu kwa wananchi na kufikia lengo la Serikali la asilimia 80 ya watanzania kuanza kutumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.






# MAFUTA GHAFI MRADI WA EACOP KUZALISHA UMEME KUKIDHI MAHITAJI WAKATI WA DHARURA

- **Mradi kutumia Megawati 100 za umeme wa TANESCO kama chanzo kikuu cha kuendeshea miundombinu.**
- **Kazi ya utandazaji nyaya za umeme ardhini kipande namba 15 kilichopo Handeni yafikia asilimia 45**
- **Mradi wanufaisha Wazawa kupitia uhaulishaji wa teknolojia kutoka kwa Wataalamu toka nje**

Mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani mkoani Tanga utazalisha umeme wake kwa kutumia mafuta yatakayozalishwa ili kukidhi mahitaji ya umeme nyakati za dharura.

Hayo yamesemwa Mratibu wa Kipande namba 15 kwenye eneo la uchomeleaji, ulazaji wa mabomba na utandazaji wa nyaya za umeme zitakazotumika kwa ajili ya vituo vya kusukuma mafuta, Mhandisi Peter Mwinuka wakati alipokuwa akizungumzia maandalizi ya ujenzi na utandazaji wa miundombinu kwa ajili ya uzalishaji wa umeme kwenye eneo la mradi ili kukidhi mahitaji ya dharura wakati wa utekelezaji wa mradi.

Amesema licha ya ujenzi wa miundombinu hiyo ya umeme wa dharura, Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania-(TANESCO), linatarajia kuipatia EACOP jumla ya megawati 100 kwa ajili ya matumizi ya umeme kwenye eneo lote la mradi kutoka vituo vya kupoza umeme vya Majani mapana, Kyaka, Kibeta, Bulyanhulu, Lusu, na Singida, ambapo kwa upande wa Umeme wa majenereta utakaozalishwa utatumia vituo vya Muleba, Igungai,Mbogwe, Singida na Tanga ambapo kila moja itakuwa na megawati 25.



Mratibu wa kipande namba 15 Mhandisi Peter Mwinuka akizungumzia maendeleo ya mradi wa utandazaji na uwekaji miundombinu ya Umeme eneo la mradi.

Akizungumzia teknolojia hiyo ya uzalishaji umeme inavyofanya kazi, Mhandisi Peter amesema kimsingi mafuta yatasafirishwa sambamba na laini 2 kutoka tilenga hadi Uganda kwa kutumia majenereta maalumu kama ilivyo kwa njia ya gridi kwa kutumia laini maalumu zizlizo sambamba na bomba la mafuta.

Amesema kwa sasa kazi ya utandazaji miundombinu hiyo ya umeme sambama na bomba imefikia asilimia 45 na kuongeza kuwa vyanzo vingine vya umeme vitakavyotumika wakati wa utekelezaji wa mradi huo ni pamoja na umeme wa jua ambapo kwa sasa wako kwenye mazungumzo juu ya utekelezaji wa mradi huo ambao utatekelezwa eneo la kambi pindi mradi utakapokamilika

Amesema kwa mujibu wa mpango kazi, wanalazimika kulaza mabomba hayo kwa takribani kilometa 3 kwa siku kama hakuna changamoto. hadi kilomita 2 mpaka 1.5 kama kuna changamoto.

Akitoa tathmini ya ushiriki wa wazawa kwenye utekelezaji wa mradi wa EACOP sambamba na manufaa kwa wazawa mmoja wa wanufaika wa mradi ambaye ni kijana David Chinanda amesena kumekuwa na mafanikio makubwa kwenye mradi huo kutokana na ujuzi kutoka kwa wataalamu



Mmoja wa wanufaika wa wataalamu kutoka nje kwenye mradi wa EACOP David Chinanda akielezea namna alivyojifunza utaalmu wa masuala mbalimbali kwenye mradi.

kutoka nje ya nchi ambao wana uzoefu mkubwa kwenye utekelezaji wa miradi kama hiyo.

Amesema hapo awali alikuwa hafahamu masuala mengi kuhusu ubora na utekelezaji wa miradi kwenye sekta ya mafuta ila kutokana na wataalamu wa nje kuwapa elimu ya ndani yeye amekuwa ni mjuzi zaidi kiasi cha kuwafundisha wengine

‘’ Kiukweli mimi sikuwa mtaalamu kabisa kwenye hii teknolojia ya kusimika mabomba ardhini ila nawashukiru hawa wataalamu kwa sasa wazawa tumenufaika na utaalamu wao na tunaweza kufanya kazi popote hata za kimataifa” Amesema David.

Ameeleza kuwa, mradi huo wa Bomba la Mafuta Ghafi umeajiri vijana wengi wenye ujuzi na wasio na ujuzi na wamekuwa wakifanya vizuri kitaaluma. Kwa upande wake mtaalamu wa masuala ya ubora na ambaye ni msimamizi wa mradi wa kipande namba 15, Mhandisi Gokhan



Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka Wizara ya Nishati, Bi Neema Chalila Mbuja akihojiwa na Shirika la utangazaji Tanzania (TBC) ziara bomba la mafuta ghafi la africa mashariki EACOP kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani mkoani Tanga.

Demircan amesema anafurahishwa na namna wazawa wanaotekeleza mradi wa EACOP wanavyojifunza kwa bidii teknolojia mbalimbali na kufanya vizuri.

Amesema vijana wengi wazawa walioko kwenye mradi wa EACOP wanaweza kuutumia ujuzi huo kwenye utekelezaji wa miradi minhine mikubwa ndani na nje ya nchi kwa kuwa ujuzi walioupata ni zaidi ya ule wa vyuo vya _mafunzo.

# DKT MATARAGIO AITAKA EACOP KUONGEZA KASI UTEKELEZAJI MIRADI YA KIJAMII KWA WANANCHI WANAOPITIWA NA MRADI

- Lengo ni kuwafanya wananchi kuwa wa mradi
- Atembelea ujenzi wa kituo namba 4 cha kusukuma mafuta Mbogwe na kambi namba 8 ya ujenzi Bukombe
- Asifu maendeleo ya mradi na kumtaka mkandarasi kumaliza kazi kwa wakati

Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Sekta ya Mafuta na Gesi Wizara ya Nishati, Dkt James Mataragio, ameelekeza kampuni ya ujenzi wa bomba la mafuta -EACOP kuhakikisha inaongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya huduma za kijamii (Csr activities) kwa kutenga fedha za utekelezaji wa miradi hiyo ili wanqnchi wanaozunguka eneo la mradi kujiona kuwa ni sehemu ya mradi

Dkt Mataragio ameyasema hayo mjini Mbogwe na Bukombe mkoani Geita wakati wa ziara yake ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki unaoendelea kwenye kipande namba 8 pamoja na kituo namba 14 cha kusukuma mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani mkoani Tanga.

“ EACOP mnapaswa kuainisha mahitaji ya kijamii ya wananchi kwenye maeneo husika kama utekelezaji wa huduma za kijamii na kwa mujibu wa matakwa ya utekelezaji wa mkataba ili wananchi wanufaike na miradi ya Maji, Barabara, Shule, Hospitali na huduma zingine za kijamii” Amesema Dkt Mataragio

Amesema kwenye maeneo



mengj EACOP imefanya vizuri, maendeleo ya mradi yanakwenda vizuri ila kwenye eneo hilo la kurudisha huduma kwa jamii wanapaswa kuliangalia upya na kuja na mpango mkakati wa utekelezaji ili jamii inayozunguka mradi inufaike zaidi.

Kwa upande wake Msimamizi wa kituo namba 4 cha kusukuma mafuta eneo la Mbogwe, Jihad Diab amesema kwa sasa EACOP inajipanga kutekeleza mkakati wa huduma za jamii CSR ili kusaidia miradi mbalimbali kwenye jamii ambapo kwa sasa wamekwisha ainisha mahitaji ya kila eneo tayari kwa utekelezaji

Amesema ili kuiweka jamii karibu na mradi, wamekuwa na programu za kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa mradi na kuwapa fursa viongozi wa vijiji kutembelea eneo la mradi na kuzungumza na wananchi mara kwa mara ili wajione ni sehemu ya mradi

Ujenzi wa bomba la mafuta kipande namba 8 eneo la Bukombe

umefikia asilimia 36 huku eneo la kituo namba 4 eneo la Mbogwe ukkfikia asilimia 46.1

Ujenzi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki unatekelezwa na nchi mbili za Tanzania na Uganda ambapo kila moja ina hisa asilimia 15, ambapo CNOOC ya China wana asilimia 8 na Total Energies asilimia 62 na mradi unatarajia kukamilika mwezi Julai, 2026.



# WANANCHI KIJIJI CHA NDEBWE WILAYA YA CHAMWINO WAPATIWA MAJIKO BANIFU 310.

- Yatolewa na Shirika la Offgridsun kuhamasisha matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia
- Mkurugenzi wa Nishati Safi ya Kupikia Wizara ya Nishati apongeza wadau kuunga mkono jitihada za Serikali
- Wananchi wapongeza

Shirika la Offgridsun wakishirikiana na Shirika la Action for Community care leo tarehe 29 Julai 2025 wamegawa majiko banifu 310 kwa wananchi wa Kijiji cha Ndebwe wilayani Chamwino mkoani Dodoma ikiwa ni uungaji mkono juhudi za Serikali katika kuhamasisha matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia.

Valentina Quaranta ambaye ni Meneja wa Mradi kutoka Action for Community Care (ACC) amesema lengo wanalokusudia ni kugawa majiko banifu 200,000 kwa wananchi ambapo mpaka sasa wameshagawa majiko 25,000 kwa mkoa wa Tanga, Morogoro pamoja na Dodoma.

Valentina Quaranta amesema majiko hayo banifu yanapunguza sana matumizi ya kuni na mkaa na hivyo kupunguza athari za uchafuzi wa mazingira.

Kwa upande wake, Nolasco Mlay, Mkurugenzi wa Nishati



Nolasco Mlay, Mkurugenzi wa Nishati safi ya Kupikia kutoka Wizara ya Nishati(watano kulia) Valentina Quaranta ambaye ni Meneja wa Mradi kutoka Action for Community Care (Wa tatu kulia) akishirikiana na wadau wengine wakikabidhi jiko banifu kwa mnufaika.

safi ya Kupikia kutoka Wizara ya Nishati amepongeza jitihada za wadau katika kuunga mkono jitihada za Serikali katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Nishati Safi ya Kupikia.

Amesema lengo la Serikali ni kuhakikisha ifikapo 2034 asilimia 80 ya wananchi wanatumia Nishati Safi ya Kupikia. Hivyo amewaomba wadau hawa kufika na maeneo mengine ili kuongeza chachu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Ametoa wito kwa wananchi wa kijiji cha Ndembwe kuhakikisha Wanayatunza majiko hayo ili kuendelea kulinda afya zao na mazingira kwa ujumla.

Wananchi wa kijiji cha Ndebwe kwa nyakatii tofauti wameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita pamoja na wadau kwa kuwapatia majiko hayo ambapo wameahidi kuyatunza.

# MRADI WA EACOP HAUNA ATHARI ZA KIMAZINGIRA; WANANCHI ZAIDI YA 26,000 WANUFAIKA NA MAJI

- Wananchi wapongeza Serikali na EACOP kuweka Sera nzuri na Teknolojia rafiki kwa mazingira
- Timu ya wataalamu wa SULUHU watembelea chanzo cha maji mto zigi kujionea maendeleo ya ujenzi wa bomba la Mafuta
- EACOP yagharamia zaidi ya shilingi Bilioni 2.728 kuwezesha Tanga Uwasa kugharamia mradi wa maji
- NEMC yapongezwa kwa usimamizi mzuri wa hifadhi ya mazingira kwenye eneo la mradi



Wananchi wakitoa shukrani zao na pongezi kwa Serikali na EACOP kwa kuweka Sera nzuri na Teknolojia rafiki kwa mazingira.

Imeelezwa kuwa mradi wa ujenzi wa bomba la Mafuta ghafi la Afrika Mashariki -EACOP hauna athari za kimazingira kutokana na Serikali kuweka Sera nzuri na Teknolojia rafiki kwa mazingira ili kulinda Bayoanuai wakati wa upitishaji wa bomba la Mradi chini ya mto zigi

Hayo yameelezwa na msimamizi wa mradi wa ujenzi wa bomba kuvuka mto Sigi kinachojumuisha ulazaji wa bomba na uchorongaji kwa ajili ya kuvusha bomba chini ya mto Mhandisi Thomas Mhando, wakati alipokuwa akielezea maendeleo ya mradi kwenye eneo hilo,sambamba na kuhakikisha mazingira yanalindwa kipindi chote cha kusimika bomba hilo

Amesema wakati wa utekelezaji wa shughuli za ujenzi wa bomba linalopita chini ya mto, suala la uhifadhi wa mazingira limepewa kipaumbele cha hali ya juu sambamba na kutoa elimu kwa wananchi juu ya utunzaji wa vyanzo vya maji hasa cha mto Zigi ,kwani ndio tegemeo kwa wananchi wa Tanga na mradi wa EACOP kwa ujumla,ambacho kinahudumia takribani watu 26,552 ambao wanapatiwa maji na mamlaka ya maji Tanga uwasa.

Ameongeza kuwa, wakati wa utekelezaji wa mradi kupeleka maji EACOP, walikubaliana kuwawezesha pia wananchi wa vijiji saba vilivyoko karibu na maeneo ya utekelezaji wa mradi kwa kuhakikisha wanapatiwa maji chini ya mradi wa makubaliano ambapo Jumla ya shilingi Bilioni 2.728 zilitolewa na EACOP kutekeleza mradi wa maji ili



Mafundi kutoka kampuni ya CPP kutoka China wakiwa wanaendelea na ujenzi wa bomba linalopita chini ya mto kwenye kipande namba 16 mradi wa EACOP.

wananchi pia wapate maji.

Awali akizungumza kwenye eneo la utekelezaji wa mradi huo mratibu wa kitaifa wa mradi kutoka TPDC Asiadi Mrutu amesema, kwa sasa uvushaji wa bomba kwenye mto Sigi unaendelea vizuri na umefikia asilimia 63 na unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2025 na ameishukuru NEMC kwa kusimamia suala la mazingira kwenye mradi huo kwa kuhakikisha wanatembelea Mara kwa mara ili kuona kazi inavyoendelea.

Kwa upande wake, Mhandisi kutoka kitengo cha Miradi Tanga Uwasa Mhandisi Aaron Chanimbaga ameishukuru EACOP kwa kuhakikisha wananchi wanafikiwa na huduma ya maji saa 24 tofauti na ilivyokuwa awali na bomba hilo Lina uwezo wa kutoa lita za ujazo milioni moja na laki



Muonekano wa utunzaji wa mazingira kwenye chanzo cha mto Sigi mkoani Tanga

saba kwa siku na linahudumia wananchi wa Chongoleani, Ndaoya, Putini, Elani,Mleni, Mabokweni,na Kibafuti.

Ameishukuru Serikali ya awamu ya sita chini ya Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa ujio wa mradi wa bomba la Mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani mkoa wa Tanga na kueleza kuwa umeleta mabadiliko ya Kiuchumi kwa mkoa wa Tanga

# MIRADI YA NISHATI SAFI IACHE ALAMA KWA WANANCHI

- Nia ni kuhakikisha Bara la Afrika linatumia nishati kwa ufanisi na kupunguza upotevu wa umeme
- Ni la pili kufanyika tangu kuasisiwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko

Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mha. Innocent Luoga amesema utekelezaji wa miradi ya nishati safi ya kupikia inapaswa kuweka alama kwa wananchi ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa



Kamishna luoga ameyasema hayo tarehe 3 julai ,2025 wakati akifungua mkutano wa sita wa kamati ya uwekezaji miradi ya nishati safi ya kupikia unaotekelezwa kwa pamoja kati ya Serikali, Umoja wa Ulaya na Shirika la umoja wa mataifa la maendeleo na mitaji ili kusaidia utekelezaji wa miradi ya nishati safi ya kupikia

''Serikali kupitia Wizara ya Nishati na wadau wa nishati safi ya kupikia imefanya kazi kubwa kuhakikisha malengo yanatimia ikiwemo utekelezaji na ushirikishwaji wa sekta binafsi kwenye miradi ya nishati safi ya kupikia ili kubadili fikra na kutimiza azma ya Serikali ya kufikia asilimia 80 ya watanzania kutumia nishati safi ya kupikia ifikapo 2034" Amesema



# WAZIRI MKUU KASSIM MAJALIWA AMEKABIDHI TUZO YA UMAHIRI KWA MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO WIZARA YA NISHATI


Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Wizara ya Nishati, Bi Neema Chalila Mbuja akipokea tuzo ya umahiri kutoka kwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa kufuatia mchango wake alioutoa wakati wa Maonesho ya Dunia ya Biashara ya Osaka nchini Japan kwa upande wa Mawasiliano na kuitangaza nchi.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa mnamo tarehe 13 Julai, 2025 amemkabidhi Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Wizara ya Nishati, Bi Neema Chalila Mbuja tuzo ya umahiri kufuatia mchango wake alioutoa wakati wa Maonesho ya Dunia ya Biashara ya Osaka nchini Japan kwa upande wa Mawasiliano na kuitangaza nchi.

Mhe Majaliwa amempongeza Bi. Mbuja wakati wa kilele cha Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es salaam maarufu kama Sabasaba 2025.

Sambamba na hilo Mhe Majaliwa amempongeza Bi. Mbuja kwa kuwa muongozaji wa shughuli na kuwa mahiri wakati wa Kongamano la Kimataifa la Biashara, Uwekezaji na Utalii kwenye Maonesho ya Osaka Expo 2025.

Kwa upande wake Bi. Mbuja amemshukuru Mhe. Majaliwa kwa kukabidhi tuzo hiyo iliyotolewa na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara TANTRADE na kuahidi kuendelea kuitangaza Wizara ya Nishati Kimataifa.



# WIZARA YA NISHATI IMEHAMIA RASMI MJI WA SERIKALI MTUMBA




Wizara ya Nishati imehamia rasmi katika Mji wa Serikali, ili kurahisisha utendaji wake wa kazi. Ikiwa ni baada ya kukamilika kwa Jengo hilo lililopo Mtumba Jijini Dodoma mwanzoni mwa Julai 2025.

**Viongozi mbalimbali wa Wizara ya Nishati pamoja na Watumishi wakiwa katika hafla ya uzinduzi wa Dira 2050 iliyofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma. Dira hiyo imezinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan mnamo tarehe 17 Julai 2025.**






















# MATUKIO KATIKA PICHA - MAONESHO SABA SABA DAR ES SALAAM



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania ( TANESCO), Lazaro Twange alipotembelea Banda la Wizara ya Nishati na Taasisi zake katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara maarufu kama SABASABA yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.












Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Usafirishaji na Usambazaji Umeme (ETDCO) CPA Sadock Mugendi alipotembelea Banda la Wizara ya Nishati na Taasisi zake katika Maonyesho ya 49 ya Sabasaba Yaliyofanyika tarehe 07 July 2025 Jijini Dar es Salaam.







Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Uthibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) Mha.Charles Sangweni mnamo tarehe 09,Julai 2025 alitembelea Banda la Wizara ya Nishati Katika Maonyesho ya 49 ya Biashara Ya Kimataifa yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam Maarufu kama Sabasaba na kujionea jinsi Wizara inavyo endelea kutekeleza Miradi mbalimbali Nchini.












Wadau na Wananchi mbalimbali walipata wasaa wa kutembelea katika Banda la Wizara ya Nishati, kwenye Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa-maarufu kama Sabasaba ili kupata elimu kuhusu Wizara ya Nishati na Taasisi zake.






# MRADI WA UJENZI WA BOMBA LA MAFUTA (EACOP) UMELETA MAPINDUZI YA KIUCHUMI KWA WANANCHI WA TANGA

- Wananchi wampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mafanikio ya ujenzi wa Mradi, wafikia asilimia 64.2
- Timu ya wataalamu wa SULUHU wakutana na Uongozi wa Mkoa wa Tanga, kueleza mafanikio ya mradi
- Ajira kwa wazawa kipaumbele cha mradi kwa asilimia 80
- Mradi watumia Bilioni 10.4 kulipa fidia kwa wananchi wa Mkoa wa Tanga

Wananchi waishio kwenye vijiji vinavyopakana na mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, EACOP wamesema Serikali ya awamu ya sita ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya kazi kubwa ya kubadili maisha ya wananchi kiuchumi kupitia mradi wa bomba la EACOP kwa kufungua fursa za kiuchumi kwenye maeneo hayo.

Wananchi hao wameyasema hayo leo 16 Julai, 2025 kwa nyakati tofauti wakati walipokuwa wakielezea mafanikio ya utekelezaji wa mradi huo na kueleza namna ambavyo maisha ya mtu mmojammoja wamefanikiwa kufuatia uwepo wa mradi wa EACOP.

" Sijawahi kuona mradi ambao umetoa manufaa makubwa ya kiuchumi na kubadili naisha ya wananchi wake kama huu wa EACOP na tunaishukuri sana Serikali ya Tanzania kukubali mradi huu kutekeleza" Alisema Bw. Loita Naftali mkazi wa kata ya Chongoleani

Amesema licha ya kujengewa nyumba, kupatiwa fedha za kujikimu kiasi cha shilingi 500,000 kwa mwezi, bado walipatiwa elimu ya ujasiriamali, Kilimo na ufugaji wa kisasa ili kuinua hali ya uchumi.



Mkazi wa mtaa wa ndaoya kata ya Chongoleani eneo la Manyungu ambae ni mnufaika wa mradi wa EACOP Bwana Loita Naftali akisalimiana na mratibu wa kitaifa wa mradi kutoka TPDC Asiadi Mrutu alipomtembelea

Naye, Kassim Mwavezo Mbega amesema tangu kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki EACOP mkoa wa Tanga umeimarika kiuchumi na mzunguko wa fedha kuwa mkubwa tofauti na ilivyokuwa hapo awali na kuongeza kuwa kwa sasa wimbi la ujenzi wa nyumba za wageni na za binafsi pamoja na taasisi za fedha umekuwa mkubwa kutokana na mkoa kupokea wageni wengi wa mradi wa EACOP.

Kwa upande wake, Mratibu wa Kitaifa wa Mradi wa EACOP kutoka TPDC Asiadi Mrutu amesema wakati wa zoezi la awali la kuwafidia wananchi hao Mradi ulitekeleza mpango maalumu chini ya taratibu za Kimataifa wenye lengo la kuwapatia elimu ya



mbalimbali ya maendeleo ikiwemo maji, umeme na wananchi mmojammoja. na kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri inayofanya utekelezaji wa miradi mbalimbali.

" Niahidi kuwa mkoa utaendelea kutoa ushirikiano kwenye utekelezaji wa mradi huu kwani viijana wengi wamenufaika na mradi wa EACOP kwa kiasi kikubwa " Alisema Bi. Amina


Amewashukuru Wizara ya Nishati kupitia TPDC kwa kuhakikisha wananchi wote wanafidiwa isipokuwa kwa wale 12 ambao wana changamoto binafsi ikiwemo za kifamilia na mirathi ambapo jumla ya shilingi Bilioni 10.4 zimetumika kulipa fidia sawa na asilimia 99.3.

ujasirimali na kuendeleza kilimo na ufugaji wa kisasa ili wajiendeshe kibiashara sambamba na elimu ya utunzaji wa fedha.

Amesema kupitia programu hii, imeboresha sana maisha yao na familia zao sambamba na upatikanaji wa ajira kwa wananchi wanaozunguka eneo la mradi.

Awali kabla ya kuzungumza na wananchi wanufaika wa mradi wa EACOP timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Nishati,na TPDC ,na TBC kwa ajili ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa EACOP na mafanikio yaliyopatikana kwa Serikali ya awamu ya sita, ilifika ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga na kupokelewa na Kaimu Katibu Tawala wa mkoa wa Tanga Bi Amina Kibunde Said na kuieleza timu hiyo kuwa mradi wa EACOP ni miongoni mwa miradi ya kimkakati na yq mfqno kitekelezwa hapa nchini kutokana na uwazi wa uendeshaji wa mradi huo.

Amesema uchumi wa Mkoa wa Tanga kwenye Wilaya zake 6 zinazopitiwa na mradi huo zimenufaika pia na miradi



Bwana Loita Naftali akiwa kwenye pikipiki ambayo ni moja ya matunda ya fidia mradi wa EACOP

# VITUO VIWILI VYA KUPUNGUZA KASI YA MAFUTA GHAFI EACOP KUJENGWA NCHINI

- Vinalenga kupunguza kasi ya Mafuta kutoka Hoima Uganda hadi Chongoleani Tanzania
- Ujenzi wafikia asilimia 50
- Mabomba ya kipenyo cha inchi 24 kutumika kusafirsha mafuta ghafi
- Wataalam wazawa waomba Serikali kuwa na data za kuwatambua pindi miradi inapotokea
- Ujenzi wafikia asilimia 50



Mafundi kutoka kampuni ya CPP kutoka China wakiwa wanaendelea na ujenzi wa bomba linalopita chini ya mto kwenye kipande namba 16 mradi wa EACOP

Jumla ya vituo viwili vya kupunguza kasi ya mafuta ghafi yanayotoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani- Tanga vinatarajia kujengwa ili kusaidia upunguzaji wa kasi ya mafuta ghafi yanayosafirishwa sambamba na kulinda miundombinu ya bomba hilo la mafuta.

Hayo yamesemwa na Mtaalamu wa Ujenzi wa Miundombinu hiyo kutoka kituo namba moja (PRS-1) inayojengwa Kata ya Kibaya, Wilaya ya Kiteto Mkoani Manyara. Mhandisi Damian Lasway, wakati alipokuwa akizungumzia maendeleo ya ujenzi wa miundombinu ya kituo hicho ambapo amesema ujenzi wa kituo umefikia asilimia 50.

Amesema ujenzi wa vituo hivyo utaenda sambamba na wa nchini Uganda, ambapo kwa hapa nchini vituo hivyo viwili vitajengwa sambamba na vile vya kusukuma mafuta vitakavyojengwa Muleba, Mbogwe, Igunga na Singida na vingine viwili vitakuwa nchini Uganda.

“ kazi hii ya ujenzi wa vituo hivi ni muhimu sana kwani mafuta yakiwa yanasafiri kutoka Uganda yanakuwa na kasi kubwa hivyo ni lazima kuwe na kituo cha kupunguza presha hiyo ya mafuta na baadae yaendelee kusafiri ” ameisema Mha. Lasway

Amesema kituo cha kwanza kitajengwa mkoani Manyara, Kata ya Kibaya, Wilaya ya Kiteto na cha pili kitajengwa Kata ya Sindeni, Wilaya ya Handeni Mkoani Tanga.

Ameongeza kuwa, Tanzania na Uganda zimefanya kazi kubwa





Baadhi ya mafundi wa kampuni ya CPP kutoka China wakiwa wanaendelea na uunganishaji wa mabomba kwenye kipande namba 16 mradi wa EACOP.

kwenye utekelezaji wa mradi huo wa bomba la mafuta ghafi kwa kuhakikisha wazawa wananufaika na ujuzi kutoka kwa wataalamu mbalimbali wa kimataifa kutoka nchi tofauti.

Akizungmzia namna wanavyonufaika na ujuzi huo, baadhi ya wazawa wanaofanyakazi kwenye eneo hilo akiwemo Rajab Rajab ambaye ni mhakiki ubora PRS-1 amesema kwa sasa uwezo wao umekua kwa kiasi kikubwa tofauti na ilivyokuwa awali wakati wanaingia kwenye mradi.

''Nina uhakika ukitokea mradi kama huu tena tutakuwa na uwezo mkubwa wa kutekeleza miradi jambo kubwa ni kwa Serikali kututambua na kuweka data za wataalamu ili zinapohitajika zipatikane kwa urahisi'' Amesema Rajab.

Naye Afisa Rasilimali Watu bi. Priscilla Baregu amesema licha ya wazawa kupewa kipaumbele kwenye utekelezaji wa mradi huu, tayari wameanza kuwatambua



Muonekano wa bomba la mafuta linavyoonekana bila kuathiri mazingira kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani- mkoani Tanga.

wafanyakazi wasio na ujuzi kwa kuwapeleka kwenye vyuo vinavyotambulika na kupatiwa mafunzo rasmi.

'' Mpaka sasa tumeshawapeleka wafanyakazi takribani 4 kwenye mafunzo rasmi na tunawagharamia kila kitu ili kutoa motisha na kuwa na weledi mpaka mradi utakapomalizika'' Amesema Bi. Priscilla.

Mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki utatekelezwa kwa vipande 16 ambapo cha kwanza kinaanzia nchini Uganda kuelekea Chongoleani Tanga.

For more info
**www.nishati.go.tz**



